

**KISWAHILI KARATASI YA PILI
MTHANI WA MWIGO
MWAKA WA PILI- 2019
MACHI 2019
MUDA: SAA 3**

MAAGIZO

1. Mtihani huu una sehemu mbili kuu . Sehemu ya A: Fasihi nay a B- Mbinu za Kufundishia
2. Jibu maswali matatu katika sehemu ya A. Swali la ushairi ni la lazima. Changua maswali mengine mawili. Moja kutoka kwa mwaya usijibu maswali mawili kutoka kwa kitabu kimoja.
3. Andika majibu yako kwenye nafasi ulizoachiwa
4. Jibu maswali yote katika sehemu ya B.

SEHEMU	SWALI	UPEO	ALAMA
A	1	15	
	2a	15	
	b	15	
	3a	15	
	b	15	
B	4	15	
	5	10	
	6	20	
	7	10	
JUMLA			

SEHEMU YA KWANZA (AL 15)

Ushairi

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali .

TELEZI

1. Mvuwa iliyonyesha, ya maradi na ngurumo
Kutwa na kucha kukesha, kunyesha pasi kipimo
Haikuwanufaisha, wenyewe kazi za vilimo
Wenyewe kazi vilimo, walifikwa na hasara
2. Mimeya waloipanda, ilitekukatekuka
Kazi ngumu walotenda, yote ikaharibika
Hawakuvuna matunda, waliyo wakiyataka
Waliyo wakiyataka, yakawa ya mbali nao

3. Wenye kuicha mvuwa, isiwatose mwilini
Baadhi yao wakawa, wakimbiliya penuni
Wengine hawakutuwa, hadi mwao majumbani
Hadi mwao majumbani, na kukomeya milango
4. Wenzangu dhhaka kando, nisemayo ni yakini
Ilibwaga kubwa shindo, mvuwa hiyo jamani
Na mijaji kwa mikondo, yakawa barabarani
Yakawa barabarani, mvuwa kwisha kunyesha
5. Kunyesha iliposiya, kukatapakaa tope
Zilijaa kila ndiya, isibakiye nyeupe
Ukawa mwingi udhiya, pa kupita zisitupe
Pa kupita zisitupe, kwa ndiya kukosekana
6. Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitiki
Bali mimi haamuwa, kwenenda japo kwa dhiki
Kumbe vile nitakuwa, ni mfano wa samaki
Ni mfano wa samaki, kuiendeya ndowana
7. Zikanibwaga telezi, sikujuwa kuzendeya
Ningekwenda kwa henezi, yasingenifika haya
Lakini tena siwezi, mwendo huo kutumiya
Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo

MWIGO 2019

Ushairi – Kuvuka si kuzuri

1.
 - a. Taja bahari zozote mbili za shairi hili ukitoa sababu (ala 2)
 - b. Eleza muundo wa shairi hii (ala 4)
 - c. Onyesha uhuru wa mshairi katika shairi hili (al.4)
 - d. Andika ubeti wanne kwa Lugha nathari (ala 4)
 - e. Mshororo wa mwisho wa shairi hili huitwa kimalizio. Taja istilahi nyingine inayoweza kutumiwa kuelezea mstari huu (ala 1)

2. TAMTHILA : UPEPO WA MVUA

Jibu swalii moja kati ya haya yanayofuata:

- (a) Uongozi mbaya ni jambo lililojikita katika tamthilia ya “ Upepo wa mvua” Dhibitisha huku ukirejelea matukio kadhaa. (ala 15)

AU

- (b) Taja au ueleze sifa tano za kila mmoja wa wahusika wafuataao. (al 15)

- (i) Waadi
 - (ii) Chifu mtoro
- Amina

3. RIWAYA: PENDO LA KARAHÀ (al 15)

Jibu maswali yote.

“Wanaowasukuma watoto wenu kwenye dawa ni hao matajiri wanaoziuza dawa, ni hao viongozi wenu. Mnawachagua nyinyi wenyewe. Mnawafanya wabunge. Mnawafanya “madisii” waona.”

MASWALI

- a. Toa muktadha wa dondo hili. (ala. 5)
- b. Taja maudhui mawili yanayojitokeza katika dondo hili. (ala. 2)
- c. Taja mbinu mbili za uandishi zinazojitokeza katika dondo hili. (ala. 2)
- d. Taja na ueleze sifa za msemaji (al 6)

AU

- e. Maudhui ya ujisadi yametawala Riwaya ya Pendo la Karaha. Thibitisha (al 15

SEHEMU YA B MBINU ZA KUFUNDISHIA (AL 55)

4. Eleza umuhimu wa kutumia nyenzo katika ufundishaji wako (al 5)

b) Wanafunzi wako wa darasa la tatu wana shida ya kutamka maneno yenyе sauti ch|sh. Taja mambo matano utakayofanya ili kutatua shida hii (al 5)

c) Onyesha utaratibu utakaofuata ili kusaidia wanafunzi wa swali 4b kuendeleza maneno hayo kwa usahihi.

5) Eleza mambo kumi utakayofanya ili kufanikisha funzo la ufahamu katika darasa la sita (al 10)

(6) Unafunza msamiati wa shambani katika darasa la nne. Eleza hatua kumi utakazofuata ili kufanikisha funzo hilo. (al20)

7) Onyesha utaratibu utakaofuata katika kufunza udogo wa majina katika darasa la tano.

(al 10)